Aina ya Tumbaku inayolimwa Tanzania

Kwa sasa, kuna aina mbili za tumbaku zinazolimwa nchini Tanzania: Aina hizi ni:

1. Tumbaku ya Mvuke (VFC), yenye mbegu za K326, RG17, ULTF10 na DDV10.

2. Tumbaku ya Moshi (DFC)

MUHIMU:

Pia kuna hali nzuri ya hewa kwa uzalishaji wa tumbaku ya hewa (Barley) katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Wanunuzi wa Tumbaku nchini Tanzania

Kuna kampuni sita (6) zilizosajiliwa na Bodi ya Tumbaku kununua tumbaku inayolimwa nchini Tanzania kupitia mfumo wa kilimo cha mkataba. Kampuni hizi ni:

1. Tanzania Leaf Tobacco Company Limited (TLTC);
2. Alliance One Tobacco Tanzania Limited (AOTTL);
3. Japanese Tobacco International Leaf Services Limited (JTI-LS);
4. Premium Active Tanzania Limited (PATL);
5. MAGEFA GROWERS LIMITED;
6. Grand Tobacco Limited;
7. JESPAN Company Limited;
8. Pachtech Company Limited; na
9. PETROBENA East Africa Limited.

Wasindikaji wa Tumbaku nchini Tanzania

Ni viwanda viwili tu vilivyosajiliwa na Bodi ya Tumbaku Tanzania kusindika tumbaku inayozalishwa nchini. Viwanda hivi ni:

1. Tanzania Tobacco Processors Limited (TTPL); na
2. Alliance One Tobacco Tanzania Limited.

TANZANIA TOBACCO BOARD

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIOMO

BODI YA TUMBAKU TANZANIA

SISI NI NANI?

(Huduma za Bodi)

Bodi ya Tumbaku Tanzania
Mtaa wa Shule, Ploti Na. 20-30 Kitalu "AC", S.L.P 61
TABORA - TANZANIA
Simu: 026 2604417
Nukushi: 026 2604417
Barua Pepe: info@tobaccoboard.go.tz
Tovuti: www.tobaccoboard.go.tz

Utangulizi

Bodi ya Tumbaku Tanzania ni chombo cha udhibiti wa zao la tumbaku kilichoanzishwa chini ya sheria ya sekta ya tumbaku Na. 24 ya 2001 (kama ilivyorekebishwa na sheria ya mazao (marekebisho mchanganyiko) Na. 20 ya 2009).

Dira

Kuwa bora katika utoaji wa huduma za udhibiti, ushauri na ukuzaji wa sekta ya tumbaku.

Dhamira

Kutoa huduma kwa wakati na ubora kwa wakulima na wafanyabiashara wa tumbaku katika suala la usajili, ushauri wa kitaalam na uwezeshaji wa mchango wa sekta binafsi katika sekta ya tumbaku kwa ukuaji bora na endelevu kwa manufaa ya sekta na nchi.

Majukumu ya Bodi

a) Kuishauri Serikali juu ya sera na mikakati ya kuboresha na kuendeleza sekta ya tumbaku nchini;
b) Kudhibiti na kusimamia ubora wa tumbaku na bidhaa za tumbaku;
c) Kukusanya, kufanya uchambuzi, kutunza, kutumia na kusambaza taarifa mbalimbali zinazohusiana na sekta ya tumbaku;
d) Kufuatilia uzalishaji na usafirishaji wa tumbaku;
e) Kuweka kanuni kwa ajili ya udhibiti wadudu waharibifu na magonjwa ya tumbaku;
f) Kuweka sheria na kanuni zinazohusu taratibu za kilimo, masoko, usafirishaji, uuzaji wa tumbaku nje ya nchi na uhifadhi wa tumbaku;
g) Kuwezesha au kusaidia uundwaji wa vyama au mashirika mengine ya wadau katika sekta ndogo ya tumbaku (ambayo itaunda jukwaa la ushauri lililodhaminiwa na Bodi) na kuratibu shughuli zao;
h) Kusimamia na kudhibiti viwango vya ubora wa tumbaku;
i) Kudhibiti na kuagiza hatua za uhifadhi wa mazingira ikiwa ni pamoja na kuepuka uharibifu wa ardhi kupitia mpango wa upandaji miti wa lazima, na matumizi sahihi ya nishati ya kuni; na
j) Kuiwakilisha serikali katika mikutano ya kimataifa inayohusiana au kushughulika na tumbaku.

Huduma Zitolewazo na Bodi

a) Usajili wa Wakulima, Wanunuzi na Wasindikaji wa tumbaku;
b) Utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima;
c) Ukaguzi wa vituo vya kuchambulia na kufungia tumbaku na vituo vya kuuzia tumbaku;
d) Kusambaza taarifa zinazohusiana na zao la tumbaku na kutoa elimu kwa wakulima;
e) Kuishauri Serikali na wadau juu ya sera na maswala ya kisekta;
f) Utoaji wa leseni na vibali kwa wafanyabiashara wa tumbaku;
g) Ukaguzi wa tumbaku inayosafilishwa nje ya nchi;
h) Mpango wa kujenga uwezo. Kwa kuzingatia mabadiliko ya mtazamo wa ubora wa tumbaku kwa wateja wa kimataifa. Bodi inatoa elimu kwa wakulima kuanzia ngazi ya chini ili kuzalisha tumbaku safi na bora inayokidhi mahitaji na matarajio ya wateja wakimataifa; na
i) Kusimamia uzingatiaji wa matumizi ya pembejeo zilizoidhinishwa, uzingatiaji wa mpango wa upandaji miti na Kanuni za Kilimo Bora.

Mwenendo wa Uzalishaji wa Tumbaku

Kiasi cha uzalishaji wa tumbaku kimekuwa kikibadilika kutoka kilo milioni 126 msimu wa 2010/2011 hadi kilo milioni 50.5 katika msimu wa kilimo wa 2017/2018.
Kushuka kwa uzalishaji kunatokana na ukweli kwamba uzalishaji unategemea mahitaji ya wanunuzi wa sasa wa tumbaku lakini wakulima wanaweza kuzalisha tumbaku hadi kilo milioni 250.
Uwepo wa viwanda vya kusindika tumbaku vyenye uwezo wa kusindika tumbaku hadi kufikia kilo milioni 140 kwa mwaka kunatoa wito kwa wanunuzi / wafanyabiashara wengi zaidi kuwekeza kwenye sekta yetu ya tumbaku.

Takwimu za Uzalishaji wa Tumbaku

MSIMU WA KILIMO	UZALISHAJI (KGS)	THAMANI YA TUMBAKU (DOLA)
2009/2010	94,243,560	213,118,148.00
2010/2011	126,624,671	176,801,222.00
2011/2012	74,239,994	135,149,031.00
2012/2013	74,180,798	135,044,741.00
2013/2014	109,986,320	242,474,463.65
2014/2015	88,275,643	160,824,734.53
2015/2016	60,934,607	129,440,708.13
2016/2017	85,860,664	132,907,886.40
2017/2018	50,522,107	82,741,836.26
2018/2019	**72,522,154.51**	101,664,705.35

Tumbaku ya msimu wa kilimo 2019/2020 masoko yake yanaendelea na mpaka kufikia tarehe 26/07/2020 jumla ya kilo 32,404,511.07 za tumbaku zimenunuliwa na thamani yake ni dola za kimarekani 45,885,861.76. Kiwango hiki ambacho kimeshanunuliwa mpaka sasa ni sawa na asilimia 56.10 za tumbaku yenye mkataba ambayo ni jumla ya kilo 57,755,669.00.